wengi huko?" Yule mtu tajiri akajilaza chini na akanyamaza kwa muda na akasema, "Nilikuwa mpumbavu kiasi gani mimi? Nimekuwa na biashara kubwa sana hapa duniani lakini kule nitakuwa fukara na maskini".

Ndugu mpendwa, usije ukawa mtu wa namna hiyo. Tengeneza urafiki na Bwana Yesu. Atakushika mkono na kukuongoza kwenye maisha ya Milele ambapo utaishi Milele na Milele kwa furaha na ushirika pamoja na Yesu na Watakatifu.

Mwombe Yesu sasa:***"Yesu, mimi ni mwenye dhambi, Nisamehe dhambi zangu, Nifanye kuwa rafiki yako. Nisaidie kuishi katika ulimwengu huu na ule ujao kwa uhakika kupitia ushirika na wewe. Amen!" (1Yohana 1:9).***


Wako, Katika Jina la Yesu,
SAJU JOHN MATHEW
Tembelea: www.sjmathew.com

Rafiki mpendwa, tupo hapa ili kukusaidia wewe kuandaa maisha yako ya milele pamoja na Yesu. Usisite kuwasiliana nasi:

***Simu:***

Pastor Moses Magembe- +255 715 283819/ 784 283818
Capt. Siyame Paul- +255 767 359993
Barua pepe: gospeldsm@gmail.com

**Gospel Campaign Center**
TAG Majumbasita,
P. O. Box 77313,
Dar es Salaam Tanzania,
East Afrika.



# Sikiliza! Msafiri!!

Mvulana mmoja alikuwa njiani kuelekea shuleni.

Hey! Kijana. Unakwenda wapi? Mzee mmoja aliyekuwa amesimama kando kando ya njia akaingilia. Alikuwa mfupi, mwenye uso mpana na kidevu kikubwa.

Niko njiani kwenda shule Baba! Mtoto akajibu.



"Ukitoka shuleni, utaenda wapi?" Yule mtu akauliza tena…

Mtoto akajibu! Nitarudi tu nyumbani niende wapi? Mtoto yule akajibu bila hata kuinua kichwa chake!

"Vema! Wewe ni shuleni nyumbani, shuleni nyumbani… kuna siku utamaliza shule, Je utakwenda wapi baada ya hapo?"

Mtoto akajibu, baada ya kumaliza masomo yangu natarajia kupata kazi nzuri na nitakuwa na ofisi yangu!

“Haya!  Itakuwa tena ofisini - nyumbani, ofisini – nyumbani… baada ya hapo utakwenda wapi tena?”

Mtoto akajibu, “Nitaoa na kupata watoto na nitawasaidia kusoma nao baadaye watapata kazi na wataoa pia…”

“Siku moja utastaafu na hatimaye itakuwaje?”

Mtoto akajibu, “siku moja nitakufa, Baba” Yule mtoto hakutaka kufikiri juu ya kifo, Lakini alijua kwamba kifo ni halisi.

Ni kweli mwanangu!  Siku moja utakufa na watoto wako watakupeleka kaburini.

Baada ya kifo utakwenda wapi? (Waebrania 9:27)

Yule mvulana akashikwa na mshangao!

Baada ya kifo?  Nini?

Yule mtu aliyekuwa amesimama pembeni mwa njia alikuwa Socrates na Mwanafalsafa aliyekuwa akiwafanya watu wafikirie juu ya umilele wao.

Ni kweli kabisa hili ni tatizo kubwa.  Mara nyingi tunasahau.  Na shetani anatufanya tusahau kuhusu maisha yetu baada ya kufa.

Maisha ni safari, na wote sisi tumeshikwa na shughuli nyingi nyingi, Lakini hakuna mafanikio yoyote.  Kila kinachoonekana mwisho wake ni kaburini.  Sayasi haina jibu juu ya kifo.  Historia pia haina cha kuandika kuhusu kifo.  Hata hivyo kaburi siyo mwisho wa yote.  Bado kuna ulimwengu usioonekana, mahali ambapo tutakutana na Mungu uso kwa uso kwa ajili ya hukumu. (Ufunuo 20:11-15)

“Je uko tayari kwa hili?  Je una hofu?”

Ni kweli tunajua kwamba hatungeweza kukutana na hukumu ya haki ya Mungu wakati tulipokuwa tukiishi maisha yasiyo ya haki na yenye dhambi wakati wote.

Leo tunazo habari njema kwako.  Yesu aliyekuja katika ulimwengu huu toka Mbinguni kutusaidia ili tuweze kwenda kwenye maisha ya Milele kwa furaha, yuko tayari kukusamehe dhambi zako na anayo furaha kukufanya wewe kuwa rafiki yake (Yohana 1:11-13).  Na kama ukishakuwa rafiki wa Yesu basi hutakuwa na haja ya kuogopa kifo (Warumi 8:1-2).  Atakushika mkono na kukusaidia kuishi maisha ya furaha katika Umilele na kuwa na ushirika naye (Yohana 14:1-3).

Hii ni mfano wa hadithi moja isemayo:  Msichana mmoja wa mtu tajiri alimwuliza baba yake wakati anakufa.  “Baba unaondoka Milele hatutakuona?” Baba akajibu, “Ndiyo mwanangu ninaogopa sana maana hutaniona tena”.  Yule msichana akauliza, “Je umepata nyumba nzuri na marafiki